Matendo ya Mitume 2

Je, Nikuzaliwa Kwa Kanisa?

Moja wapo ya tamaduni za kanisa ya kisasa nikuwa Matendo ya Mitume 2 ndipo “kanisa” linazaliwa.

Hii inabakia kuwa msingi mkuu katika imani ya Kikristo katika makanisa tofauti tofauti. Utamaduni huu unatumika Kwa upana na hata kukita mizizi yakwamba hakuna maswali yanayoulizwa kuhusiana na utamaduni huu. Kwa kweli, kuuliza maswali kuhusu kuhalalishwa kwa utamaduni huu inaalika kupingwa au hata kukataliwa kama mojawapo ya dini huru potovu.

Neno “Kanisa” inapatikana katika sura za kwanza ya Matendo ya Mitume na sisi, watu wa mataifa ambao ni waumini wa sasa, tukiwa tumeamini yakwamba kuna “ Kanisa moja tu ambalo ni la kweli”, tunajiingiza katika hali hiyo, nakuongeza katika neno la Mungu mambo ambayo hayapo (Eisegeses).

Wakristo wengi hulinganisha Israeli kwa kanisa lakini hili pia ni kuchanganyikiwa kwa sababu inaulinganisho ambao si sawa. Israeli ni kundi ambalo limaitwa na Mungu kwa kusudi Fulani na pia kurithi ; Israeli ni kanisa.

Sisi waumini wa sasa, ikijumuishwa na wayahudi pamoja na watu wa mataifa waliokoka wanajumulisha kundi lingine au kanisa liitwalo kanisa ambalo ni mwili wa Kristo. Hivyo tunafaa kulinganisha hizi mbili kwa kuzichambua kama kanisa la Israeli na kanisa ambalo ni mwili wa Kristo. Israeli ni kama “kanisa la Mungu” na kama mwili wa Kristo, kwa hivyo tuna makundi mawili tofauti, na urithi mbili tofauti na kusudi mbili tofauti kwaajili ya Mungu. Kuchanganya haya mawili pamoja inachukuwa nafasi na kuleta ajali ya kitheologia.

Matendo ya Mitume 2 inakamilisha sherehe iliopewa wanaIsraeli (Law.23) na haihusishi sisi waumini wa sasa. Kwa kutojali utofauti kati ya hizi kanisa mbili tunabadilisha kile Mungu amepeana kwa Israeli kuwa kitu ambacho tumefikiria wenyewe.

Kutamadunisha pentecote ya kiyahudi kwa siku ya kuzaliwa ya watu wamataifa, tunaunga mkono uongo huu kwa kuendelea na uongo mwingine.

Kwa hivyo lazima tuwahusishe wanamataifa kwa Matendo ya Mitume 2 ilituendeleze mambo ya uongo ya kwamba wayahudi na watu wamataifa walibatizwa kwa mwili wa Kristo.

Katika somo hili tutatazama neno la Mungu ilikutambua kama hizi tamaduni za kale nisawa kiroho. Lakini kwanza tutazame kwa undani mwanzo wa pentecote.

Baadhi ya wale wanaofuata tamaduni yakwamba kanisa lilianza siku ya pentecote walitambua yakwamba wanafunzi awaigizi au kunena kwa usawa pamoja na tamaduni zao. Ilikupitisha mambo haya ambayo ni kinyume, wanasema yakwamba wanafunizi hawa labda walikuwa wamechanganyikia kuhusiana na sherehe ya pentecote ama hawakujua kabisa mwanzo mpya ambao Bwana alikuwa akitarajia kuufungua machoni pao.

Ilikuongezea hadithi zisizo za kweli kwenye uongo huu wanayochambua kama y akuhuzunisha na kundi lisilo timilika ambao hatimaye walijulishwa kuhusu kusudi la Mungu wakati Roho Mtakatifu aliwapa kufahamu. Lakini je hii mawazo na mengine sawa na hii ni ya kweli?

Kitabu cha Matendo ya Mitume kiliandikwa na Luka mtakatifu na sura ya mwisho ya injili yake na sura ya kwanza ya Matendo ya Mitume inatupa mwangaza kwa wakati huo. Hapa ni baadhi ya mistari kutoka kwa kitabu cha Luka mtakatifu 24 ambapo Bwana wetu Yesu Kristo amejithirihisha mwenyewe kwa wale wawili waliyekuwa wakielekea Emmaus na baadaye kwa wanafunzi wengine, na katika hali hizi mbili alihakikisha mambo kadhaa kwao;
Yesu akawambia, “Ninyi ni wajinga kiasi gani, nanyi ni wazito mioyoni mwenu kuamini mambo yote

yalionenwa na manabii! Je, haikumpasa Kristo kuteswa kwa njia hiyo na kuingia katika utukufu wake?” Naye akianzia na Musa namanabii yote, akawafafanulia jinsi maandiko yalivyosema kumhusu yeye. Luka 24:25-27

Akawambia, “ haya ndio yale niliyowambia nilipokuwa bado niko pamoja nanyi, kwamba yote yalioandikwa kunihusu mimi katika torati ya Musa, manabii na zaburi hayanabudi kutimizwa.” Luka 24:44

Mkombozi aliyefufuka aliwatiya moyo yakwamba lazima kuvumilia mateso kabla ya utukufu lakini hakusema yakwamba mateso yalifuatiwa nakusudi mpya kabisa pamoja na utukufu tofauti.

Kuteseka kwote kulikuwa agano la kale na utukufu ambao ulifuatiya ilitabiriwa katika agano la kale. Hii inafaa kuanza kututayarisha kujuwa utukufu ulikuwa msingi wa agano la kale nailihusisha sherehe ya pentecote na tarumbeta iliyofuata.

Utukufu ya agano la kale ni utukufu wa Mesia akija kwa tarumbeta (kutoka 19) nakutawala kwenya kiti cha kifalme baba yake Daudi kutoka Zayuni. Kwa njia nyingine, utukufu wa agano la kale sio utukufu wa kanisa ambalo ni mwili wake katika mbingu; ila ni utukufu wa ufalme mbinguni duniani.

Baada ya Israeli kuwekwa kando kama taifa mwisho wa kitabu cha Matendo ya Mitume, Paulo aliandika katika Waefeso kuhusu mambo yaliyo husisha kanisa ambalo ni mwili wa Kristo, navitu hivyo vilikuwa “avitafutiki” na vilifichwa katika Mungu” havikupatikana kwa mfano ama kwa unabii, tazama Waefeso 3:8-9.

Tukirudi kwa Luka 24 tunapata Bwana Yesu mwenyewe akijirudia baada yakuonyesha wanafunzi mikono yake na miguu na akala mbele yao. Alirudia yakwamba alikuwa amenena kuhusu kuteswa na utukufu uliokuwa umeandikwa kwenye agano la kale; utukufu wa Mungu uliokaa kati ya wana Israeli katika mlima mtakatifu. Lakini kabla ya utukufu, Mesia angeteseka kwa ajili ya wokovu wa watu wote sio ti wana Israeli. Kasha Mwokozi akafanya kitu kizuri kuwajili yao, alifungua fahamu zao iliwaelewe maandiko.
Ndipo akufungua fahamu zao iliwaweze kuyaelewa maandiko Luka 24:45.

Mawazo ya wanafunzi yalifunuliwa iliwaweze kuelewa yale maandiko ambayo Bwana Yesu aliyatumia ilikufafanua utukufu ambao ungekuja. Je, nijambo la hekima kwa mtu yeyote kusema yakwamba wanafunzi walikuwa na huzuni, wasio timilika na waliochanganyikiwa wakati alipowaagiza

wangoje ahadi ya Baba? Kwa kinyume wanafunzi walielewa upya kwa njia tofauti, ahadi yenye nguvu na baraka za Bwana wao.

Walipomtazama akipaa juu waliambiwa atarudi tena (Turumbeta) na hivyo walijawa na furaha, wakimsifu Mungu katika hekalu la Israeli, hawakujificha nyumbani wakiwa wenye huzuni na kuchanganyikiwa: **Alipokuwa anawabariki, akawaacha, akachukuliwa mbinguni kisha wakamwabudu na kurudi Yerusalemu wakiwa wamejawa na furaha kuu. Nawo wakadumu ndani ya hekalu wakimtukuza Mungu. Amen. Luka 24:51-53**

Tunarudia, wanafunzi awakukataliwa na kuchanganyikiwa, au kutokuwa na hakika kwa yale yaliyokuwa tayari kutendeka lakini walijawa na furaha tele, katika hekalu wakimsifu na kumbariki Mungu.

Mbona huu mwanzo ni wa maana? Kwasababu kama tamaduni inawanyoshea kidole cha lawama wanafunzi kwa kuyachukulia mambo isiyo faa lakini neno la Mungu linahakikisha yakwamba walikuwa sawa, basi lazima tutazame tena mambo kwa mtazamo tofauti.

Tafadhali tuplia mbali mafundisho ambayo yanatilia mkazo makosa ya kimitume.

Sura unaofungua Matendo ya Mitume inatupatia dhirihisho zaidi yakwamba wanafunzi hawakuwa wasiotilia maanani kusudi la Mungu au wenye kuchanganyikiwa.

Tumekwisha kuona yakwamba Bwana alifungua kuelewa kwao ilikuelewa maandiko pamoja na uwezo wa kiungu wa kuelewa mambo ambayo yangetokea, pia walifunzwa naye Mungu kwa zaidi ya mwezi mmoja; **Katika kitabu changu cha kwanza nilikuandikia mpendwa Theofilo, kuhusu mambo yote Yesu alifanya na kufundisha tangu mwanzo, hadi siku ile alichukuliwa kwenda mbunguni, baada ya kuwapa maelekezo kwa njia ya Roho Mtakatifu wale Mitume aliowachaguwa. Baada ya mateso yake, alijionyesha kwao na kuwathibitishia kwa njia nyingi kwamba yeye yu hai. Katika muda wa siku arobaini baada ya kufufuka kwake aliwatokea na kunena kuhusu Ufalme wa Mungu. Wakati mmoja alipokuwa pamoja nao, aliwapa amri hii “Msitoke humu Yerusalemu, bali ingojeni ahadi ya Baba, ambayo mmenisikia nikisema**

habari zake. Yohana aliwabatiza kwa maji, lakini baada ya siku hizi chache mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu.” Matendo 1:1-5

Pentecote likuwa siku ya 50 wakati wa matoleo ya sherehe ya mikate isiyotiwa chachu. Siku arobaini kati ya hizo Bwana alinena nao kuhusiana na mambo ya Ufalme wa Mungu. Ufalme wa Mungu kama inavyo patikana katika sheria ya Musa, manabii na zaburi.

Hakuna jambo lolote katika agano la kale kuhusu kikundi cha waumini walioinuliwa na kuketi pamoja na Kristo katika mbingu.

Baada ya siku arobaini, wanafunzi walikuwa na swali moja tu na haikuwa inahusiana kwa vyovyote na utukufu wa agano la kale ila tu kwa wakati;
Mitume walipokuwa wamekusanyika pamoja, wakamwuliza Yesu, “je, huu ndio wakati wa kuwarudishia Israeli ufalme?” Matendo 1:6

Tunaweza kutowa maoni kwa ujasiri kuhusu makosa ya kitume wakati Bwana mwenyewe alifunguwa kuelewa kwao kasha akanena kwao kwa siku arobaini?labda tutie alama uwezo wa mafundisho ya Bwana na alama ya kwa kukosea ama kukubali makosa yamekuwa yetu.

Lazima tusimame na neno la Mungu. Wanafunzi walikuwa sawa wakati walimwuliza Bwana kama angerejesha ufalme wa Israeli wakati ule. Ingelikuwa furaha kuu kama waKristo wangesifu wanafunzi badala ya kuwashutumu. Sasa, wacha tumsikilize Petero akiwahubiria ndunguze, watu wa Israeli;
“sasa ndugu zangu.najuwa yakuwa ninyi mlitenda bila kujua, kama walivyofanya viongozi wenu. Lakini kwa njia hii Mungu alitimiza kile ambacho alikuwa ametabiri kwa vinywa vya manabii wake wote, kwamba Kristo atateswa. Tubuni basi mkamgeukie Mungu, ili dhambi zenu zufutwe, ili zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwepo kwake Bwana. Kwamba apate kumtuma Kristo, ambaye amewekwa kwa ajili yenu, yaani Yesu, ambaye ilimpasa mbungu zimpokee mpaka wakati kufanywa upya kila kitu, kama Mungu alivyosema kwa vinywa vya manabii wake wote watakatifu kabla ya mwanzo wa ulimwengu” Matendo 3:17-21

Je injili hii inakiri mwanzo wa jambo jipya na iliyofichwa katika Mungu hapo awali?

Au je nilazima tukubali yakwamba hii injili imenenwa na Mtume akili zake zikiwa zimefunuliwa ili kuelewa maandiko ambayo yalikuwa yamenenwa kimbele kuhusu urejesho wa kifalme na kutiwa nguvu kwa Roho Mtakatufu juu ya Israeli wakati mfalme wao alirudi katika kutawala juu yao. Pentecote inatazamia mambo hayo yote.
Haturejeshi kitu kwakuleta jambo jipya au tofauti.

Petero alikuwa akitazamia wakati " burudisho" au huisho waIsraeli na wakati wa " urejesho" ambao manabii walinena kuhusu. Manabii walinena kuhusu urejesho wa kanisa ambao ni mwili wa Kristo ambao haukuweka awali, tazama Waefeso 3. je, inawezekanaje jambo ambalo halikuwepo awali kurejeshwa?

Sasa tunaangazia utamaduni yakwamba ilikuwa uzao wa kanisa kwasababu Wayahudi ama wamataifa, kulingana na vile iliaminika walibatizwa kwa mwili wa Kristo wakati Roho Mtakatifu alipomwagwa. Tumeshaona yakwamba wazu ili ni la kigeni kwa unabii kuhusiana nakuja kwa Roho Mtakatifu na urejesho waIsraeli. Lakini tunapatia mandiko nafasi ya kudhibitisha yakuwa utamaduni hauna msingi, kwa upande mwingine hakukuwa na wanamataifa wakati wa Pentecote wakuunganishwa na wayahudi; majuto nikwamba utamaduni huo hauna msingi wa Kibibilia.

Pentecote ni mojawapo ya sherehe iliyopewa waIsraeli na ilipeana kivuli ya jambo kwa taifa. Mungu aliwapa wanaIsraeli amri kuhusiana na sherehe na hii ni ya maana kwa mtazamo huu.
Wanaume wenu wote lazima wajitokeze mara tatu kwa mwaka mbele za BWANA Mungu wenu mahali atakapochagua:kwa ajili ya sikukuu ya Mikate isiyotiwa chachu, sikukuu ya majuma na sikukuu ya vibanda. Hakuna mtu atakayejitokeza mbele ya BWANA mikono mitupu: Kumbukumbu 16:16

Jerusalem ilijawa na watu waliosafiri huko kwaajili ya shughuli za kidini, kwa utiifu wa amri za Mungu walikuwa huko kwa ajili ya pasaka na pentecote. Luka anataja haya katika kifungo cha pili na tunaona kwa utaratibu watu hawa walikuwa wayahudi na waongofu, nasiyo wamataifa;
Basi walikuwepo Yerusalemu wayahudi wanaomcha Mungu kutoka kila taifa chini ya mbingu. Wakiwa wameshangaa na kustaajabu wakauliza, "Je, hawa wote wanaozungumza si Wagalilaya? Imekuwaje basi kila mmoja wetu anawasikia wakinena kwa lugha yake yakuzaliwa? Warparathi, Wamedi, Waelami, wakazi wa Mesopotamia,

Uyahudi, kapadokia, Ponto Asia, Frigia, Pamfilia, Misri na pande za Libya karibu na kirene na wageni kutoka Rumi, (Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu sote tunawasikia watu hawa wakisema katika lugha zetu wenyewe, mambo makuu ya ajabu ya Mungu." Matendo 2:5, 7-11

Mara mbili katika kifungo hiki tunaelezwa yakwamba umati wa watu ulihusisha Wayahudi pamoja waongovu kutoka mataifa kumi na mbili pamoja na sehemu zingine ambao walikusanyika kwaajili ya sikukuu. Tafadhali tambua waongovu wakutambuliwa kama mataifa na Waisraeli, wakiwa wamebatizwa, kutahiriwa, walitowa dhabihu sawasawa na masharti yao "kuzaliwa mara ya pili" pia wanachambuliwa kama waliojitolea ambapo ulikuwa ni ukweli kwa kugharimika walitii amri za Mungu ya kusimama mbele yake; pentecote ilitarajiwa na umati mkubwa wa watu kwa Waisraeli katika Tarumbeta.

Kuhakikisha kwamba umati huo ulikuwa Waisraeli peke yao tunaoredhesha njia ya kuhutubu ambaye Petero aliutumia waka alipohubiri injili yake;
Ndipo Petero akasimama pamoja na wale Mitume kumi na mmoja, akainua sauti yake na kuhutubia ule umati wa watu, akasema Wayahudi wenzangu na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, jueni jambo hili mkanisikilize. Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno haya nisemayo: Yesu wa Nasareti alikuwa mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa miujiza, maajabu na ishara, ambao Mungu alitenda miongoni mwenu kwa kupitia yeye, kama ninyi wenyewe mjuavyo. Ndugu zangu Waisraeli, nataka niwaambie kwa uhakika kwamba Baba yetu Daudi alikufa na kuzikwa, nalo kaburi lake lipo mpaka leo. Kwa hiyo Waisraeli wote na wajue jambo hili kwa uhakika kwamba: Mungu amemfanya huyu Yesu, ambaye ninyi mlimsulubisha, kuwa Bwana na Kristo. Matendo 2:14, 22, 29, 36

Na katika sura ya tatu.
Petero alipoona watu wamekusanyika akawaambia, "Enyi waume Waisraeli, kwa nini mnastaajabu kuhusu jambo hili? Mbona mnatukazia macho kwa mshangao kana kwamba ni kwa uwezo wetu au utakatufu wetu tumefanya mtu huyu kutembea? Ninyi ndio wana manabii na wa agano ambalo Mungu alifanya na baba zenu, akamwambia Abrahamu, katika wewe, jamaa zote za duniani watabarikiwa." Matendo 3:12, 25

Hakuna mtu wamataifa ambaye ni Mwisraeli au ndugu wa kimwili wa Petero au katika sehemu yeyote katika nyumba ya Israeli au mwana wa Baba wa Israeli. Kama watu wa mataifa ni watu waliobadili imani na kumjua Mungu basi yeye sio mtu wa mataifa tena.

Kufikia hapo tumetowa kwenu sababu mbili za kimandiko kwanini hakukuwa na watu wamataifa katika umati huo wakati wa sikukuu ya pentecote. Lakini ilikuwa vigumu kuthibitisha.

Katika Matendo ya Mitume sura ya kumi mtume Petero alikuwa safarini kuelekea Joppa. Alikuwa mwenye njaa na akapata usingizi mzito sana kasha akaona maono. Katika maono haya aliona shuka ikishuka toka mbinguni mara tatu ndani mwake mlikuwa na wanyama wa kila aina. Sauti ikamwambia inuka uchinje kisha ule;
Alipokuwa akiomba akaona, na akatamani kupata chakula. Lakini wakati walikuwa wakiandaa akalala usingizi mzito sana. Ndani yake walikuwepo aina zote za wanyama wenye miguu manne, nao watambaao na ndege za angani. Ndipo sauti ikamwambia "Petero, ondoka, uchinje na ule." Matendo 10: 10-13

Mtume alikataa sauti kutoka mbinguni kwa msingi wa kutazama sheria kwa uaminifu. Petero alikuwa Mwisraeli ambaye alizingatia sana sheria;
Petero akajibu, "La Bwana! Sijakula kamwe kitu chochote kilicho najisi." Matendo 10:14

Tafadhali zingatia maneno " kawaida na unajisi." Ni sheria gani ambayo ingeingia katika mawazo ya Petero wakati wa maono haya ambayo yalimfanya kujibu kwa maneno kawaida au unajisi? Maono ya wanyama bila shaka kutazamia sheria waliopewa Waisraeli kuhusu vyakula;
Kwa hiyo, ninyi lazima mweze kutofautisha kati ya wanyama walio safi na wasio safi pia kati ya ndege wasio safi na walio safi. Msijitie unajisi kutokana na mnyama yeyote au ndege wala kitu cho chote kitaambacho juu ya ardhi, vile ambavyo nimevitenga kuwa najisi kwa ajili yenu. Mtakuwa watakatifu kwangu, kwa sababu mimi BWANA, ni mtakatifu, nami nimewatenga kutoka katika mataifa kuwa wangu mwenyewe. Law 20:25-26

Chakula cha Waisraeli ilikuwa iwe ukumbusho kwa Wayahudi kwamba Mungu hakuwa na hasira kwao kutoka kwa Wamataifa lakini haikumanisha yakwamba Wamataifa hawangeokolewa kama Petero alivyonena katika

Matendo 3:26. Petero alikuwa karibu kupokea wmaliko kutoka kwa Wamataifa lakini Israeli haikuwa imerejeshwa.
Wacha msomaji ahakikishiwe yakuwa bila hii maono na bila sauti kutoka mbinguni, Petero angelikataa mwaliko kwa kubagua na kumwambia Mungu kwamba " haliwezekani Bwana", tazama Matendo 11:17. hakuna chochote kama sio sauti ya Bwana inyoweza kubadilisha mawazo ya mwanadamu;
Ile sauti ikasema naye tena mara ya pili, "usikiite kitu cho chote alichokitakasa Bwana." Matendo 10:15

Ni nini ambalo aliumba kuwa safi (Yohana 1:29) na Petero asiite yakawaida? Taarifa ifatayo iliyotolewa na Petero kwa Kornelio inaunganisha maoni haya kwa uwazi na Wamataifa ambao hadi sasa walihesaboka na Petero kuwa wakawaida na wasio safi;
Akawambia, " Mnajuwa kabisa kwamba nikinyume cha sheria yetu Myahudi kuchangamana na mtu Mmataifa au kumtembelea. Lakini Mungu amenionyesha kwamba nisimwite mtu ye yote kuwa najisi au asiye safi. Matendo 10:28

Hadi Matendo kumi Petero aliamini "ilikuwa kinyume na sheria" kwa Misraeli kuwa na ushirika na Wamataifa wasio safi. Hakukuwa na Wamataifa wakati wa pentecote kama sivyo ilikuwa na haja gani Petero kuoneshwa cho chote? Je, Bwana baada ya miaka mingi kupita angefunza Petero jambo ambalo alikuwa anajua?

Petero anaendelea kusema "lakini Mungu amenionesha." Ni lini Mungu alimuonesha Petero yakwamba Wanamataifa wasiitwe " wakawaida au najisi"? Sio wakati wa pentecote lakini wakati wa maono katika Matendo 10. wakati tamaduni inawaweka Wamataifa katika Matendo 2 inakatalia mbali ukweli wa Matendo 10:11-18. Je Petero anachukuliwa kwa makosa tena au utamaduni zetu zimetufanya vipofu?

Petero alipokea sehemu tatu ya maono kabla ya wanaume hao watatu kufika na mwaliko kutoka kwa Wamataifa na wakati mwaliko ulitolewa Petero alipokea hakikisho, wakati huu kutoka kwa Roho Mtakatifu;
"Wakati ule ule watu watatu, waliokuwa wametumwa kutoka kaisaria waliwasili katika nyumba niliyokuwa nikikaa. Roho Mtakatifu akaniambia niende nao bila kuwa na ubaguzi kati yao na sisi. Hawa ndugu sita pia walifuatana nami , nasi tukaingia nyumbani mwa huyo Kornelio". Matendo 11:11-12

Bwana akamwambia Petero yakwamba asiwaite Wamataifa wakawaida au wasio safi alikuwa amewaosha. Kasha Roho Mtakatifu akathibitisha maneno ya Mungu kwa kumelezea Petero yakwamba asiwatenge kwahivyo Petero alikwenda nyumbani kwa Kornelio na akauliza swali nzuri;
Ndiyo sababu ulipotuma niitwe nilikuja bila kupinga lo lote. Basi sasa naomba inieleze kwa nini umeniita". Matendo 10:29

Mwanafunzi Wakikristo wa bibilia, hili swali la Petero lazima lisababishe uwaze. Mbona ammulize Mmtaifa Kornelio kile alichotaka kama Petero alikuwa tayari amekwisha wahubiria Wamataifa katika Matendo 2? Naomba ya kwamba tayari umekwisha uliza swali lililo wazi. Kwa nini Petero alihitaji sehemu tatu ya maono ili kwenda kwa Wamataifa kama tayari walikuwa wamebatizwa katika " kanisa" katika Matendo 2? Je Petero hakuamriwa kwenda katika dunia?

Nakama vitu hivi havitoshi basi weka jambo nzuri kutoka katika Matendo 11;
Mitume na ndugu walioamini waliokuwa huko Uyahudi wakasikia kuwa watu wamataifa nao wamepokea neno la Mungu. Matendo 11:1

Je lini Mitume na wandugu walisikia yakwamba Wamataifa pia walipokea neno la Mungu? Matukio haya ni mwaka mingi baada ya Matendo 2. Je hawa Mitume na wandugu walikuwa wamechanganyikiwa tazama jinsi wanavyoonekana wajinga kwa sababu ya tamaduni? Tazama jinsi tunavyo simama kinyuma na maandiko? Tunaweza kuwaita waliokosea wakati tamaduni zetu ndizo zenye makosa?

Iliyojumulishwa kati ya wandugu ilikuwa ni kundi la walio tiwa tohara na Petero;
Hivyo Petero alipopanda Yerusalemu, wale wa tohara waliokuwa wameamini wakamshutumu, wakisema, " kwa nini ulikwenda kwa watu wasiotahiriwa na kula pamoja nao?" Matendo 11:2-3

Kwa nini kikundi hiki kilimenyana na na Petero kama Wamataifa walikuwa wamebatizwa katika "kanisa" katika Matendo 2? Kwa nini walingangana na Petero kama kweli Wamataifa walikuwa tayari wakwisha "ndelea katika ushirika, na kuumega Mikate nyumba kwa nyumba" pamoja na Wayahudi?

Petero anaelezea matukio kwa upana na anamalizia na maneno haya;

Nami nilipoanza kusema, Roho Mtakatifu akashuka juu yao kama vile **alivyotushukia sisi hapo mwanzo. Basi ikiwa Mungu aliwapa hawa watu kipawa kile kile alichoyupa sisi tuliomwamini Bwana Yesu, mimi ni nani hata nifikirie kuwa ningeweza kumpinga Mungu? Matendo 11: 15, 17**

Kama tungelitaka thibitisho la mwisho yakwamba Wamataifa hawakuwepo wakati wa pentecote ndio hii sasa. Petero ananena yakwamba Kornelio alipokeya Roho Mtakatifu kama vile Waisraeli pale mwanzo, ambaye ni pentecote.

Mungu alimpa Kornelio kipawa, labda Petero angejaribu kumzuia Mungu bila maono. Tena Petero angenena vipi kama Wamataifa walikuwa tayari wamebarikiwa katika Matendo 2?

Mitume na wandugu pia walitambua;
Waliposikia haya hawakuwa na la kupinga zaidi. Nao wakamwadhimisha Mungu wakisema, “Basi, Mungu amewapa hata watu Mataifa toba iletayo uzima wa milele.” Matendo 11:18

Katika Matendo 10 na 11vikundi vitano au watu binafsi wanatuhakikishia yakwamba hakukuwa na Wamataifa katika Matendo 2.

1. Bwana mwenyewe, ambaye alimpa Petero maono kuhusu kujumulishwa kwa Wamataifa.
2. Roho Mtakatifu ambaye alimwambia Petero asiwabaguwe .
3. Petero mwenyewe, ambaye angekataa kwenda kama hangepewa amri iliyo eleweka.
4. Kikundi cha waliotiwa tohara.
5. Wale Mitume wengine na wandugu ambao hatimaye walitambua yakwamba Mungu alikuwa katika haya..

Katika vinywa vya mashahidi wawili au watatu jambo litathibitishwa lakini hadi sasa, ingawaje taarifa kutoka kwa neno, tamaduni ya Wakristo uliendelea kushikilia upotovu. Je wote walikuwa hai na kuhusishwa katika matukiyo haya walipotoshwa au je ni tamaduni zetu zilizopotevu? Hapakuwepo na Wamataifa katika Matendo 2 walioitaji kubatizwa katika mwili wa Kristo. Pentecote ni sherehe za Kiyahudi inayounganishwa na ufalme kutoka mbiguni mbaka duniani.

Katika kijitabu hiki umeonesha yakwamba Israeli ni kundi lililoitwa na utukufu ambao Bwana alinena na kufundisha wanafunzi wake, ulikuwa ni utukufu uliopo duniani wa agano la kale.
Pia tulitambua wanafunzi walijawa na furaha na mawazo yao kufunguliwa ili kuelewa maandiko katika agano la kale. Ahadi ya agano la kale kuhusu Roho Mtakatifu ilipatikana katika kifungo ambaye ilinena kuhusu urejesho wa utukufu wa Waisraeli na hivyo swali ya wanafunzi katika Matendo 1:6 ilikuwa sawa.

Pentecote ilikuwa ni sherehe iliyopewa Waisraeli na katika hiyo sherehe Roho Mtakatifu alipeana vipawa vya Roho Mtakatifu kwa Wayahudi na waongovu peke yao. Miaka mingi baadaya Petero alitumwa kwa Mtaifa baada ya maono kati yao wawili. Hatua ya Petero, waliokuwa pamoja naye na wale waliowachwa Yerusalemu inadhirihisha ya kwamba Matendo 2 sio kuzaliwa kwa kanisa bali kutimilishwa kwa sherehe ya kanisa Israeli.

Wanafunzi hawakuwa waliochanganyikiwa na wasiojali; walijuwa pentecote inahusu nini, ilikuwa kuhusu Waisraeli na ufalme wake uliokuwa inakuja duniani. Waisraeli walibakia kuwa watu wa Mungu hadi kufungwa kwa kitabu cha Matendo. Katika barua ya Paulo alituma barua ya Matendo kwa Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, Tito, Filemoni na waraka wa 1 na 2 Timotheo tunasoma kuhusu kanisa ambalo ni mwili wake na utukufu katika mbigu.

Kwa maelezo zaidi;
www.bibleunderstanding.com
kageuni2005@yahoo.com
pstrsym6f@yahoo.com
bibleunderstanding@yahoo.com
charis9@netzero.net